JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

WIZARA YA UCHUKUZI

# MAMLAKA YA HALI YA HEWA TANZANIA

## TAARIFA YA HALI MBAYA YA HEWA KWA MWEZI MACHI NA APRILI, 2025

### 1.0 UTANGULIZI

Katika kipindi cha miezi ya Machi na Aprili, 2025 mvua ziliendelea katika maeneo mengi ya nchi sambamba na ongezeko kidogo la mvua katika baadhi ya maeneo. Hali hii ilisababisha ongezeko la unyevu ardhini, kina cha maji na malisho kwa baadhi ya maeneo, lakini pia mafuriko na kutuama kwa maji katika maeneo mengine. Hali ya joto nyakati za mchana ilijitokeza katika maeneo yaliyokuwa na upungufu wa mvua hususan yale yanayopata misimu miwili ya mvua kwa mwaka katika kipindi cha mwezi Machi na kuathiri shughuli zinazofanyika maeneo ya nje/wazi. Kwa upande mwingine, vipindi vya upepo mkali vilijitokeza katika maeneo ya ukanda wa Pwani, Ziwa Victoria na nyanda za juu kaskazini mashariki. Hali ya hewa iliyojitokeza pamoja na athari zake imeendana na taarifa za mwelekeo wa mvua za msimu zilizotolewa hapo awali.

### 1.1 Mvua kubwa kwa mwezi Machi, 2025


Katika kipindi cha mwezi Machi, 2025 vipindi vya mvua vilijitokeza katika maeneo mengi nchini. Aidha, vipindi vya mvua kubwa pamoja na ngurumo vilijitokeza katika baadhi ya maeneo nchini na kusababisha mafuriko, uharibifu wa mali, na kuathiri shughuli za kiuchumi. Kiwango cha juu zaidi cha mvua cha milimita 135.8 kilirekodiwa katika kituo cha Karema (mkoa wa Katavi) mnamo tarehe 19 Machi, ikifuatiwa na milimita 129.4 katika kituo cha Mtwara mnamo tarehe 11 Machi na milimita 117.0 katika kituo cha Zanzibar mnamo tarehe 28 Machi, 2025. Vituo vilivyoripoti vipindi vya mvua kubwa vya milimita 50 au zaidi ni kama vinavyoonekana kwenye Kielelezo 1.

*Mawasiliano yote yaelekezwe kwa:*
Mkurugenzi Mkuu, Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania, Chuo Kikuu cha Dodoma,
Jengo la Utawala, Ndaki ya Sayansi za Kompyuta na Elimu Angavu, 1 Mtaa wa CIVE,
S.L.P 27, 41218 Dodoma; Simu: +255 26 2962610: Nukushi: +255 26 2962610

Barua pepe; met@meteo.go.tz; Tovuti: www.meteo.go.tz

**(IMETHIBITISHWA – ISO 9001:2015, Huduma za Hali ya Hewa kwa Usafiri wa Anga)**

*728G _ 01/2023*




**Kielelezo 1:** Vituo vilivyoripoti viwango vya mvua kubwa kwa mwezi Machi, 2025.

Kutokana na mvua zilizokuwa zikiendelea kunyesha, taarifa kutoka katika vyombo vya habari zilithibitisha kutokea kwa athari mbalimbali katika baadhi ya maeneo nchini. Athari hizo ni pamoja na uharibifu wa mali na miundombinu ambayo inaweza kuhatarisha maisha ya watu..



**Kielelezo 2**: Daraja katika Mto Nyamli katika Kijiji cha Bugarama Wilaya ya Maswa lililofungwa kutokana na kuhatarisha maisha ya watu kufuatia mvua zilizokuwa zinaendelea kunyesha katika Mkoa wa Simiyu (Chanzo: *Gazeti la Mwananchi*)..

## 1.2 Hali joto kwa mwezi Machi, 2025

Katika kipindi cha mwezi Machi 2025, hakuna ripoti ya vipindi vya baridi kali vilivyorekodiwa nchini. Aidha, kiwango cha chini zaidi cha joto cha nyuzi joto 12.1 °C kilirekodiwa katika kituo cha Igeri (mkoa wa Njombe) kwa siku 2 ndani ya mwezi.

Kwa upande mwingine, hali ya joto ilijitokeza katika baadhi ya maeneo nchini, hususan yale ya mwambao wa pwani na nyanda za juu kaskazini mashariki. Hali hii ilipelekea kuathiri shughuli zinazofanyika nje na maeneo ya wazi nyakazi za mchana. Hali ya joto zaidi ilirekodiwa katika kituo cha Mlingano (mkoa wa Tanga) ikiwa na kiwango cha juu zaidi cha nyuzi joto 37.3 °C kilichorekodiwa mnamo tarehe 13 Machi 2025. Aidha, kituo cha Mlingano kilirekodi viwango vya joto la juu ya nyuzi joto 35 °C kwa siku kumi (17) kwa kipindi cha mwezi Machi.

**Jedwali 1**. Idadi ya siku ambazo viwango vikubwa vya joto la juu vilijitokeza kwa mwezi Machi, 2025

| Kanda | Kituo | Idadi ya siku (≥ 35°C) | Kiwango cha juu cha joto ($^{0}$C) |
|---|---|---|---|
| Nyanda za juu kaskazini mashariki | Kilimanjaro | 5 | 36.2 °C |
| | Moshi | 5 | 36.5 °C |
| Pwani ya Kaskazini | Mlingano | 17 | 37.3 °C |
| | Zanzibar | 2 | 35.4 °C |
| | Dar | 5 | 36.9 °C |
| | Morogoro | 3 | 35.5 °C |
| | Kibaha | 8 | 36.3 °C |
| | Tanga | 2 | 35.2 °C |
| Ukanda wa ziwa Victoria | Mwanza | 1 | 35.5 °C |

## 1.3 Upepo Mkali kwa mwezi Machi, 2025

Katika kipindi cha mwezi Machi, 2025 vipindi vya upepo mkali unaofika kilomita 40 hadi 50 kwa saa vilijitokeza katika baadhi ya maeneo nchini ikiwemo ukanda wa pwani (Mkoa wa Dar es Salaam, Pwani, Tanga, Lindi, Mtwara na visiwa vya Unguja na Pemba) na maeneo machache ya nyanda za juu kusini magharibi (mikoa ya Rukwa na Songwe).


Nguvu ya upepo ilisababisha athari mbalimbali ikiwemo kusambaa kwa vumbi, kupeperushwa kwa takataka na kusababisha kupungua kwa uono. Maeneo machache ya mwambao wa pwani ya bahari yalipatwa na vipindi vya mawimbi makubwa na

kuathiri baadhi ya shughuli zinazofanyika baharini sambamba na kuhatarisha jamii zinazofanya shughuli mbalimbali katika maeneo ya mwambao wa pwani.

### 1.4 Mvua kubwa kwa mwezi Aprili, 2025

Katika kipindi cha mwezi Aprili, 2025 vipindi vya mvua zilizoambatana na radi vilijitokeza katika maeneo mengi, hususan maeneo yanayopata misimu miwili ya mvua kwa mwaka. Aidha, vipindi vya mvua kubwa vilijitokeza katika baadhi ya maeneo na kusababisha mafuriko, uharibifu wa miundombinu na mali, na kuvuruga baadha ya shughuli za kiuchumi. Mnamo tarehe 27 Aprili, 2025 kituo cha Pemba kilipima milimita 136.1 za mvua kwa saa 24 ikiwa ni kiwango cha juu zaidi ikifuatiwa na milimita 94.8 katika kituo cha Matangatuani mnamo tarehe 11 Aprili na milimita 91.5 katika kituo cha Mbozi( mkoa wa Mbeya) mnamo tarehe 5 Aprili.

Vituo vilivyoripoti vipindi vya mvua kubwa vya milimita 60 au zaidi ni kama vinavyoonekana kwenye Kielelezo 3.




**Kielelezo 3:** Viwango vya mvua kubwa kwa mwezi Aprili, 2025

Ripoti kutoka vyombo vya habari zimethibitisha uwepo wa athari mbalimbali zilizotokana na mvua zilizonyesha mwezi Aprili. Barabara kuu ya kutoka Dar es Salaam kwenda mikoa ya kusini ilikatika kufuatia mvua kubwa iliyonyesha tarehe 6 Aprili, 2025. Kutokana na hali hiyo, mawasiliano ya usafiri yaliathiriwa kwa kiasi kikubwa nabaadhi ya madaraja kusombwa na maji, ikiwemo daraja la Somanga–Mtama na daraja la Mto Matandu (*Chanzo: Gazeti la Mwananchi*).



**Kielelezo 4:** Basi la abiria likivuka kwa tahadhari njia ya muda huku mawasiliano ya usafiri kati ya Somanga na Mtama yakianza kurejea taratibu (*Chanzo: Gazeti la Mwananchi*).

### 1.5 Hali joto kwa mwezi Aprili, 2025

Katika kipindi cha mwezi Aprili 2025, hali ya joto kiasi ilijitokeza katika baadhi ya maeneo yanayopata misimu miwili ya mvua kwa mwaka, hususan maeneo ya ukanda wa pwani. Katika kipindi hiki hakukuwa ripoti ya joto kali nchini. Kiwango cha juu zaidi cha nyuzi joto 34.4 °C kilirikodiwa katika kituo kilichopo uwanja wa ndege wa kimataifa wa Mwl. Julius Nyerere (JNIA) mnamo tarehe 9 Aprili, 2025.

### 1.6 Upepo Mkali kwa mwezi Aprili, 2025

Vipindi vya upepo mkali unaofika kilomita 40 hadi 50 kwa saa vilijitokeza katika baadhi ya maeneo nchini ikiwemo ukanda wa pwani (Mikoa ya Tanga, Dar es Salaam, Pwani, Lindi, Mtwara pamoja na Visiwa vya Unguja na Pemba) na ukanda wa ziwa Victoria (mikoa ya Mwanza na Kagera). Nguvu ya upepo mkali ilisababisha athari mbalimbali katika maeneo hayo.

*Matukio haya ya hali mbaya ya hewa yanaonesha ongezeko la changamoto zinazosababishwa na mabadiliko ya hali ya hewa na tabianchi na umuhimu wa kutekeleza mikakati thabiti ya kukabiliana mabadiliko hayo ili kulinda jamii na mazingira*.

*Imetolewa: tarehe 15 Mei, 2025*
**Na Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania.**

*Mawasiliano yote yaelekezwe kwa:*
Mkurugenzi Mkuu, Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania, Chuo Kikuu cha Dodoma,
Jengo la Utawala, Ndaki ya Sayansi za Kompyuta na Elimu Angavu, 1 Mtaa wa CIVE,
S.L.P 27, 41218 Dodoma; Simu: +255 26 2962610: Nukushi: +255 26 2962610

Barua pepe; met@meteo.go.tz; Tovuti: www.meteo.go.tz

**(IMETHIBITISHWA – ISO 9001:2015, Huduma za Hali ya Hewa kwa Usafiri wa Anga)**

*728G _ 01/2023*